# CHUO KIKUU CHA DODOMA

## NENO FUPI KUTOKA KWA MKUU WA CHUO MHESHIMIWA BALOZI MHANDISI JOHN W.H. KIJAZI KATIKA MAHAFALI YA 11 YA CHUO KIKUU CHA DODOMA SIKU YA TAREHE 17 DESEMBA, 2020 KATIKA UKUMBI WA CHIMWAGA

**ITIFAKI**

- ***Mheshimiwa Philip Isdor MPANGO (Mb.), Waziri wa Fedha na Mipango;***

- ***Mheshimiwa Omari Juma KIPANGA (Mb.), Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia;***

- ***Mheshimiwa Mama Gaudentia Mugosi KABAKA, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo;***

- ***Mheshimiwa Balozi Charles SANGA, Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo;***

- ***Mheshimiwa Mama Anna MKAPA na Familia ya Hayati Mheshimiwa Benjamin Mkapa;***

- ***Dkt. Leonard AKWILAPO, Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;***

- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;***

- ***Bwana Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge la Tanzania;***

- ***Wajumbe wa Baraza la Chuo;***

- ***Prof. Faustine BEE, Makamu Mkuu wa Chuo;***

- ***Prof. Alexander MAKULILO, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma;***
- ***Prof. Donald MPANDUJI, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utawala;***

- ***Maprofesa, Wahadhiri na Wanataaluma wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma;***

- ***Viongozi mbalimbali wa Serikali mliopo;***

- ***Wafanyakazi na Wanafunzi wote wa Chuo;***

- ***Wahitimu mnaoshiriki katika Mahafali ya 11 ya Chuo Kikuu cha Dodoma;***

- ***Waandishi wa Habari;***

- ***Wageni waalikwa wote, mabibi na mabwana.***

- ***Habari za Mchana!!***

**<u>UTANGULIZI NA SHUKRANI;</u>**

***Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma;***

Awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuweza kutukutanisha mahali hapa siku ya leo, tukiwa na afya njema kwa ajili ya tukio la Mahafali ya 11 ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kipekee kabisa, natoa shukrani zangu nyingi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuniamini na hivyo kuniteua katika nafasi hii ya Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Nimeupokea uteuzi huu kwa unyenyekevu mkubwa, na ninaahidi kwamba nitashirikiana kikamilifu na Viongozi wengine wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma katika kuhakikisha kuwa Chuo hiki kinafikia malengo yake yaliyowekwa.

***Ndugu Viongozi, Jumuiya ya Wanachuo na Wageni Waalikwa;***

Sote tunatambua kwamba, Chuo Kikuu cha Dodoma kilimpoteza Mkuu wa Chuo wa kwanza na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Hayati Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ambae alifariki dunia mnamo tarehe 23 Julai, 2020. Kifo chake kilikuwa ni msiba mkubwa, sio tu kwa

Chuo Kikuu cha Dodoma, bali pia kwa familia yake na kwa Taifa na Dunia kwa ujumla. Kwa niaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma, natoa pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa na Familia yote ya Hayati Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwa msiba mkubwa walioupata. Nawaomba tusimame kwa dakika moja ili kutoa heshima zetu na kumkumbuka Hayati **Mheshimiwa Benjamin William MKAPA**. **(Kusimama Dakika Moja).** *Raha ya Milele Umpe Ee Bwana, na Mwanga wa Milele Umuangazie. Apumzike kwa Amani Mheshimiwa Benjamin William* Mkapa. Hakika sisi sote ni wa Mungu, na kwake tutarejea.

***Ndugu Viongozi, Jumuiya ya Wanachuo na Wageni Waalikwa;***

Takriban wiki tatu zilizopita, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi mwingine wa Kiongozi muhimu kwa ajili ya Chuo chetu Kikuu cha Dodoma. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa **Gaudentia Mugosi KABAKA** kwa kuteuliwa kwa mara ya pili na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 24 Novemba, 2020 kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo. Ni dhahiri kuwa, utendaji wake mzuri wa kazi hii katika kipindi chake cha kwanza, ndio umewezesha kuaminiwa na kuteuliwa tena kwa mara nyingine ili kuendelea kushika nafasi hii. Hongera sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo chetu, na tunautegemea sana uongozi wako mahiri katika kipindi cha miaka minne ijayo.

***Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo,***

Napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Viongozi, na Jumuiya ya Wanachuo kwa namna mlivyonipokea tangu siku ya kwanza nilipokuja kujitambulisha hapa Chuoni mnamo tarehe 29 Septemba, 2020 hadi leo. Pia, nawapongeza kwa kuendelea kutekeleza majukumu yenu kwa bidii, weledi na maarifa. Tayari nimeshafanya ziara ya kutembelea baadhi ya Ndaki, na nimeshajifunza mambo mengi na kuona uhodari wenu na vilevile nimeshazifahamu baadhi ya changamoto zinazokikabili Chuo chetu ambazo inabidi tuzitafutie ufumbuzi.

Kwa muhtasari, katika Ndaki nilizozitembelea nimejionea na kuridhika jinsi ambavyo Chuo kinaendesha programu mbalimbali zenye

kuhitajika katika Taifa letu, ambazo zinalenga katika kuzalisha Wataalamu watakaokabiliana na changamoto mbalimbali zinazolikabili Taifa. Aidha, programu hizo pia zinatoa mafunzo yenye viwango vya ubora vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Napenda kuuhakikishia Uongozi mzima wa Chuo kuwa nitaendelea kushirikiana nanyi ili kuwezesha Chuo chetu kiendelee kutoa Wahitimu wenye viwango vinavyotambulika na kukubalika Kimataifa.

Nitaendelea kutembelea Ndaki zilizobaki kabla ya mwishoni mwa mwezi Januari, mwaka 2021 ili niendelee kujifunzaa kuhusu mafanikio na changamoto za Ndaki hizo.

*Ndugu Viongozi na Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;*

Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru ninyi wote kwa kuwepo kwenu hapa siku ya leo ili kushuhudia Mahafali ya Kumi na Moja ya Chuo Kikuu cha Dodoma, ambayo yameambatana na shughuli kuu **tatu**:

(i) Shughuli ya **kwanza** ambayo imekamilika tayari ni kusimikwa kwa Mkuu wa Chuo mpya. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo pamoja na Uongozi wote wa Chuo, nawashukuru sana kwa namna mlivyoendesha zoezi zima la kunisimika katika nafasi hii ya Mkuu wa Chuo, na hivyo basi kukamilisha utaratibu wa kuniingiza rasmi katika Jumuiya ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Asanteni sana.

(ii) Shughuli ya **pili** ni kutunuku Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kwa Hayati Mheshimiwa **Benjamin William MKAPA,** tukio ambalo litafuata hivi punde;

(iii) Na shughuli ya **tatu** ni kuwatunuku wahitimu mbalimbali vyeti vya **Astashahada**, **Stashahada**, **Shahada**, **Stashahada za Juu**, **Shahada za Umahiri**, na **Shahada za Uzamivu**. Nawapongeza sana Wahitimu wote kwa ufaulu na kufikia hatua hii ya kutunukiwa Shahada zenu leo. Lakini pia natoa pongezi zangu kwa Maprofesa, Wahadhiri na Wanataaluma

wengine wote pamoja na Wafanyakazi wote wa Chuo kwa michango yenu muhimu iliyowezesha kuwapata wahitimu hawa.

***Ndugu Viongozi, Watumishi na Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma,***

Kabla sijamaliza maelezo yangu, napenda kusisitiza kuhusu umuhimu wa Chuo chetu kuwa na mazingira rafiki yanayowezesha malengo ya msingi ya chuo kufikiwa kwa ufanisi. Hivyo, mnao wajibu wa kuhakikisha kuwa changamoto zilizo ndani ya uwezo wa Chuo zinapatiwa ufumbuzi mapema. Nawakumbusha Viongozi, Watumishi na Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kuzingatia taratibu sahihi za mawasiliano zilizowekwa na Chuo katika kushughulikia changamoto za Watumishi na Wanafunzi. Kwa kufanya hivyo, na endapo kila mhusika atatekeleza wajibu wake ipasavyo, basi hakuna sababu ya kuwepo kwa migogoro baina ya Wafanyakazi, Wanafunzi na Uongozi wa Chuo. Tujenge utamaduni wa kumaliza changamoto zilizo ndani ya uwezo wetu kwa kuheshimu na kutumia taratibu za Chuo tulizojiwekea.

Nafurahi kwamba Uongozi wa Chuo umenihakikishia kuwa milango yao ipo wazi ili kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi changamoto za Wanafunzi pamoja na Wafanyakazi wa Chuo. Hivyo, hakuna sababu ya kukimbilia kwa Viongozi ama kwenye Ofisi za nje ya Chuo kwa masuala ambayo yanaweza kumalizika ndani ya Chuo.

Kwa upande wa Wahitimu ambao mtatunukiwa Vyeti vya kumaliza na kufaulu masomo yenu, nawatakia kila la heri na mafanikio katika maisha yenu yanayofuata, na nendeni mkawe Mabalozi wazuri wa Chuo chetu, kwa kwenda kutekeleza vizuri majukumu yenu mbalimbali ya kulijenga Taifa kupitia fani mlizosomea. Katekelezeni majukumu hayo kwa **juhudi, maarifa, weledi na kujiamini**, iwe kwa kujiajiri wenyewe ama kwa kuajiriwa kaatika Sekta ya Umma au Sekta Binafsi.

## HITIMISHO

*Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo;*

Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza la Chuo na Uongozi wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kusimamia na kuendeleza Chuo chetu. Nawaahidi kwamba, tutafanya kazi kwa pamoja na kwa ushirikiano mkubwa ili kuhakikisha kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kinatekeleza kwa ufanisi majukumu yake ya msingi ya kutoa **Elimu Bora ili kuzalisha nguvukazi bora inayohitajika kwa ajili ya kuwezesha maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu, pamoja na kufanya Tafiti zitakazowezesha utatuzi wa matatizo mbalimbali kwa manufaa ya Taifa letu.**

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Mungu ibariki Tanzania, na Mungu kibariki Chuo Kikuu cha Dodoma.

**Imetolewa na:-**
*Mheshimiwa Balozi* Mhandisi John W.H. Kijazi,
**MKUU WA CHUO**,
Chuo Kikuu cha Dodoma,
**17/12/2020**